

# Mreno kava watu 3

Mwafrika

13-9-63

**W**ATU watatu wameuliwa na askari wa Kireno huko Msumbiji baada ya watu hao kugunduliwa kwa-mba ni wanachama wa FRELIMO. Mmoja miongoni mwa watu hao alikuwa ni mwanamke'

Habari hizi zimetangazwa leo mjini Dar es Salaam na Katibu wa Habari katika ofisi Kuu ya FRELIMO, Bw. Chiteji.

Alisema kwamba mtu wa kwanza ambaye jina lake haljulikani ni wa kijiji cha Kunuma. Yeye baada ya habari kufikishwa katika Mtwala wa Kireno wa wilaya ya Mueda kwamba anayo kadi ya chama cha siasa.

Askari watatu walitumwa kumkamata; na baada ya kufikishwa Bomani aliadhihiwa vikali na askari wa Kireno.

Akiwa taabani mtu alipeleka ndani ya jela ambako alikufa baada ya muda mfupi.

Mwanamke ambaye naye ameuawa kwa njia ya mateso kama hayo ya mtu wa kwanza anaitwa Tresa Munda, ambaye alikuwa na umri wa mlaka 22.